# CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA

# RIPOTI YA UCHAMBUZI NA USHAURI KUHUSU BAJETI KUU YA SERIKALI YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**MACHI, 2021**

## 1. Shukrani

THTU kama wadau wakubwa wa maendeleo katika kufikia uchumi thabiti unaofungamanisha maendeleo ya watu imeandaa uchambuzi wa bajeti ya nchi kwa mwaka wa fedha 2021/22 ili kuisaidia serikali, na mihimili mingine ikiwemo bunge na wadau wa maendeleo katika kuchochea maboresho ya uandaaji wa bajeti pamoja na utekelezaji thabiti ili kuongeza tija katika kuimarisha na kukuza uchumi wenye kuboresha maisha ya watanzania wakiwemo wafanyakazi.

Kwa niaba ya Uongozi, shukrani za dhati ziende kwa wanajumuiya wote na wanachama wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu (THTU), kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kuishauri serikali katika kuimarisha mifumo ya utekelezaji wa majukumu yake. Kipekee kabisa, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa kamati maalum ya uchambuzi wa bajeti iliyohusisha wataalamu wanachama kutoka taasisi za elimu ya juu wakishirikiana na uongozi wa THTU Taifa katika mchakato wa kuchambua bajeti na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuboresha bajeti ya nchi hasa katika kukusanya mapato na kuboresha mifumo ya utekelezaji wa bajeti. Kamati hii iliundwa na Dkt. Paul Loisulie (THTU Makao Makuu), Ndg.Elia Kasalile(THTU Makao Makuu), CPA Aisha Kapande (THTU Makao Makuu), Ndg. Ngussa Kinamhala-CP3P (LGTI), Dkt. Deo Shao (UDOM), CPA David Mwakapala (UDOM), Ndg. Salatiel Chaula (OUT), Ndg.Imani Haule (UDOM) na Wakili Khery Sanga (LST).

Vilevile tunatoa shukrani zetu kwa wadau wote walioshiriki katika kutoa maoni yao juu ya uandaaji wa taarifa hii. THTU inathamini na kutambua michango na maoni yaliyotolewa katika kushiriki kikamilifu kwenye ujenzi wa taifa ili kufikia malengo yanayotarajiwa.

**© Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), 2021**
Sehemu yoyote ya Ripoti hii inaweza kunakiliwa kwa matumizi yasiyo ya kibiashara, kwa sharti kwamba chanzo kitatambuliwa na nakala mojamoja ya chapisho itatumwa kwa THTU.

Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU) S.L.P 35928 DAR ES SALAAM, Tanzania

Simu: 022 2401581, Nukushi: 022 2401582

Wavuti: www.thtu.or.tz, Barua pepe: thtuhq@gmail.com

## 2. Muhtasari

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ilianza kutekelezwa mwaka 2000 ili kuongoza harakati za maendeleo ya kiuchumi na kijamii zitakazoiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa kati na kuondokana na umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2025. Ili kutimiza malengo hayo, serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali zikiwemo za kuandaa mipango na mikakati ya utekelezaji wa dira ya Taifa ya Maendeleo. Lengo la kuandaa mipango na mikakati yote ni kuhakikisha serikali inaendelea kuboresha viashiria muhimu vya uchumi, ikiwa ni pamoja na kuchochea ukuaji wa pato la taifa, kuimarisha sarafu/ shilingi ya nchi, kudhibiti mfumuko wa bei, kuimarisha mazingira ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuvutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi, kuongeza ajira kwa wananchi hasa kundi la vijana pamoja na kufungamanisha sekta mbalimbali za kiuchumi na maendeleo ya watu.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2016/17 – 2020/21) serikali imefanya juhudi katika kutafuta mbinu mbadala za kuongeza na kuimarisha mazingira ya kukusanya pato la ndani. Hata hivyo, ufanisi wa makusanyo upande wa Serikali za Mitaa umekua duni, ambapo wastani wa kipindi cha miaka mitatu iliyopita ni asilimia 79 tu ya makusanyo yalipatikana ikilinganishwa na lengo lililowekwa. Sambamba na hilo, malipo ya mishahara ya wafanyakazi yamekuwa hayafikii malengo kwa kipindi cha miaka mitano. Kutofikia lengo la bajeti eneo hili kunaibua malimbikizo mapya yanayoongeza deni la serikali la ndani na kupelekea jumla ya deni la nchi kufikia asilimia 7.6% kwa mwaka 2020/21. Sambamba na hilo, eneo la mifumo inayosaidia kuongeza ufanisi wa kukusanya mapato ya aina tofauti ya serikali limeonekana linakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo kutokuwepo kwa mifumo thabiti yenye ufanisi kwenye ngazi zote.

Katika kuboresha ufanisi wa makusanyo ya mapato ya nchi, THTU inaishauri serikali kupitia bajeti ya 2021/22 iendelee kutoa kipaumbele kwenye sekta zinazofungamanisha uchumi wa viwanda na maedeleo ya watu katika kuboresha sekta za kijamii; serikali kuendelea kuchukua hatua za kisera, kiutawala na kiutendaji kurejesha biashara zilizoathirika moja kwa moja kutokana na janga la Korona pamoja na sekta tanzu zinazotegemea shughuli za kibiashara; Kuboresha mfumo tangamani wa matumizi (framework of adoption) ya TEHAMA katika serikali ili kuwa na ufanisi zaidi; kujenga uwezo wa ndani katika kuunda na kuratibu mifumo ya serikali hasa inayohusiana na mapato; Kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mifumo ya TEHAMA inayohusiana na ukusanyaji na usimamizi wa kodi; Kuweka mikakati ya kuboresha kanzidata ya huduma, bidhaa sambamba na taarifa za walipa kodi; Serikali ielekeze nguvu katika kuchochea viwanda vinavyotumia malighafi nyingi za ndani zinazotokana na mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi; na Kuendelea kurasimisha sekta zisizo rasmi na kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kupata vyanzo vipya vya mapato.

Mwisho, THTU inaamini kwamba, mapendekezo haya pamoja na ya wadau wengine yakifanyiwa kazi kwa umakini, mapato yataongezeka na hivyo serikali itakuwa kwenye nafasi nzuri ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kuongeza kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 270,000 kilichopo sasa hadi kufikia shilingi 360,000; pamoja na kutenga katika bajeti ya nyongeza ya mishahara ya mwaka (Annual Increments) kwa wafanyakazi ili kuboresha zaidi maisha yao kama ambavyo serikali imeendelea kuonyesha kusisitiza wakati wote juu ya suala hili.

## 3. YALIYOMO

Shukrani ........ ii

Muhtasari ........ iv

1. Utangulizi ........ 1

2. Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na Mipango ya Taifa ya Maendeleo Katika Kufikia Uchumi wa Kati ........ 2

3. Sera, Mwenendo na Tathmini ya Bajeti ........ 4

4. Uboreshaji wa Mifumo ya Ukusanyaji Kodi katika Kuongeza Uwezo wa Serikali Kimapato 6

5. Mapendekezo ya THTU juu ya namna bora ya kutekeleza sera ya viwanda na namna itakavyosaidia kuboresha maslahi ya wafanyakazi. ........ 8

6. Maoni katika kuboresha bajeti ya Serikali ........ 9

6.1. Kuongeza wigo wa kodi ........ 9

6.2. Kupunguza changamoto zinazohusiana na mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. ........ 11

6.3. Usimamizi na ukaguzi kwenye kampuni ambazo Serikali ina hisa ........ 11

6.4. Miradi ya Serikali za Mitaa ........ 11

7. Mapendekezo juu ya Kodi ya Mapato ya Ajira (PAYE) ........ 12

9. Mfanyakazi na mfumuko wa bei. ........ 14

12. Hitimisho ........ 23

13. Rejea na Bibliografia ........ 25

**Orodha ya Majedwali**


Jedwali Na. 1: Utozaji kodi kabla ya mwaka wa fedha 2020/2021 ............................................ 12

Jedwali Na. 2: Utozaji kodi kwasasa ............................................................................ 12

Jedwali Na. 3: Mapendekezo ya utozaji kodi baada ya Mabadiliko .......................................... 13

Jedwali Na. 4: Ada za huduma ya Bandari ..................................................................... 13

Jedwali Na. 5 : JAda za Michezo ya kubahatisha ............................................................... 13

Jedwali Na. 6: Mfumuko wa bei ............................................................................... 14


## Orodha ya Vielelezo


Kielelezo Na. 1 : Uhusiano wa Bajeti na Malipo Halisi ya Mishahara ......................................... 5

Kielelezo Na. 2: Farihisi za Bei ............................................................................... 16

Kielelezo Na. 3 Makadirio ya Mapato ya Ndani .................................................................. 17

Kielelezo Na. 4 : Makisio ya Matumizi ......................................................................... 18

## 4. Vifupisho vya Maneno

| | |
|---|---|
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CPA | Certified Public Accountant |
| CP3P | Certified Public Private Partnership Professional |
| FYDP | Five Years' Development Plan |
| GePG | Government electronic Payment Gateway |
| ILO | International Labour Organization |
| LESCO | Baraza la Kazi la Jamii na Uchumi |
| LGTI | Local Government Training Institute |
| LST | Law School of Tanzania |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| OUT | Open University of Tanzania |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| THTU | Tanzania Higher Learning Institutions Trade Union |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| UDOM | University of Dodoma |
| VAT | Value Added Tax |

## 5. Dibaji

Hii ni mara ya pili THTU inafanya uchambuzi wa bajeti kuu ya serikali ili kushauri vyanzo vya mapato na matumizi inayolenga kumnufaisha mfanyakazi na wadau wengine. Mara ya kwanza ilikuwa ni mwaka 2019 tulipochambua mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020. Katika mara hii ya pili, tumeona dibaji ya mara ya kwanza bado inafaa na hatuna haja ya kuandika upya. Hivyo, tunarejea ile dibaji ya mwanzo bila kubadili chochote.

Vyama vya wafanyakazi huanzishwa ili kujenga na kuendeleza mahusiano baina ya mwajiri na mwajiriwa. Chama cha wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu Tanzania (THTU) kimeanzishwa kisheria kutetea uboreshaji wa maslahi mbalimbali ya wafanyakazi katika taasisi hizo. Utetezi huu unafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu, miongozo na nyaraka mbalimbali za serikali au taasisi husika. Kauli mbiu ya THTU ni hii: Nia na Mwelekeo wetu daima ni Kujenga, Taifa Kwanza.

Kihistoria, uanzishwaji wa vyama vya wafanyakazi umejikita katika harakati zaidi na hivyo kujenga sura ya kutoaminiana kati ya mwajiri na wafanyakazi katika utekelezaji wa maslahi ya wafanyakazi. Mabadiliko ya kisheria, kimfumo na kimuundo yamekuwa yakitokea katika uendeshaji wa vyama hivi na kupelekea kupungua kwa utamaduni wa kutoaminiana uliokuwepo awali.

Kutokana na mabadiliko hayo tajwa, uanzishwaji wa THTU umejielekeza katika kuboresha mbinu za kutetea maslahi ya wafanyakazi. Kauli mbiu yetu imebuniwa kwa lengo la kutoa muelekeo mpya na mbinu za kisayansi katika kutetea maslahi ya wafanyakazi. Mbinu za kisayansi ni kufanya utafiti na kuonesha kitakwimu na kiuhalisia katika kujenga hoja pamoja na kuishauri serikali namna bora ya kuimarisha uchumi na hatimaye kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Sheria za Tanzania zimeweka utaratibu mzuri wa kuongoza uendeshaji wa vyama vya wafanyakazi na namna ya kuwasiliana na mwajiri. Mfano wa taratibu hizo zilizowekwa kisheria ni pamoja na majadiliano kazini, uanzishwaji wa mabaraza ya wafanyakazi na uwakilishi wa wafanyakazi katika vyombo vya maamuzi kwa kutaja machache. Kutokana na kauli mbiu ya THTU, tunaona tuna deni kubwa katika taifa hili kutoa mchango wetu kwa ustawi wake na kupata maendeleo endelevu na hatimaye sisi wafanyakazi kunufaika moja kwa moja.

Ni kwa msingi huo ulioelezwa hapo juu, THTU inaona ina wajibu wa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa hili katika kufikia malengo yanayotarajiwa kwa wakati. Kauli mbiu hii inatuhamasisha sisi THTU kuwa washirika wa maendeleo na si watazamaji. Hii maana yake ni kwamba tukishiriki kikamilifu katika kukuza pato la taifa, na sisi wafanyakazi tunafaidika moja kwa moja maana ni washirika. Katika dhana ya ushirika katika maendeleo, kila upande una kitu cha kuchangia kwa manufaa ya pamoja.

Jambo moja muhimu la kuweka bayana ni kwamba THTU ina hazina kubwa ya wanachama wenye viwango na weledi mkubwa wa elimu waliobobea katika nyanja mbalimbali. Ili kufikia azma ya kutetea uboreshwaji wa maslahi ya wafanyakazi, THTU imeunda kikosi kazi cha kufanya uchambuzi wa namna bora ya kutambua maslahi ya wafanyakazi kupitia bajeti kuu ya serikali ya mwaka 2021/2022. Uchambuzi umejikita zaidi katika masuala yote yahusuyo uandaaji wa bajeti yakiwemo sera, sheria kanuni na miongozo mbalimbali, vyanzo vya mapato, uwiano wa mapato na matumizi kisekta na mengine. Lengo kuu la uchambuzi huu ni kupendekeza njia nzuri ya kumnufaisha mfanyakazi bila kuathiri mwenendo mzima wa uendeshaji wa nchi.

## 1. Utangulizi

Katika utaratibu wa uwajibikaji wa nchi yoyote duniani, wanazuoni wanaohusika na masuala ya Utawala na Uongozi wamebainisha makundi matatu ya watu kwenye mgawanyo wa majukumu. Mgawanyo huu wa majukumu umekaa katika mfumo wa pembe tatu. Kundi la kwanza ni wananchi (umma) ambalo ndilo kundi kuu na ndio msingi wa uwepo wa nchi husika. Kundi hili la kwanza ndilo lenye mamlaka na madaraka yote ya nchi. Kundi la pili ni wanasiasa ambao huzaliwa au hutokana na kundi la kwanza. Kundi hili ndilo linalokasimiwa mamlaka na madaraka na wananchi (umma) ili kuweza kubuni, kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma zote za kijamii na kiuchumi zinazohitajika kwa umma. Kwa hiyo, wanasiasa huwajibika kwa wananchi (umma). Kundi la tatu ni la wafanyakazi ambalo huzaliwa au hutokana na wanasiasa. Kundi hili la tatu huajiriwa na wanasiasa kwa ajili ya kutekeleza mipango yote ya utoaji wa huduma kwa wananchi (Umma) kwa maelekezo ya wanasiasa. Kundi hili ni la wataalamu wa fani mbalimbali wanaohusika katika utoaji wa huduma kwa umma. Kundi hili huwajibika kwa wanasiasa.

Maelezo yaliyotolewa hapo juu yanadhihirisha kwamba kundi la tatu ambalo ni wafanyakazi (wataalamu) ndio nguzo kuu inayotumika kutekeleza mipango ya utoaji huduma za kijamii na uchumi. THTU kama kielelezo cha kundi la tatu ina utajiri mkubwa wa wataalamu wa fani karibu zote zinazohitajika katika utekelezaji wa mipango ya utoaji huduma. Kwa msingi huu na kwa kuzingatia kauli mbiu ya THTU isemayo nia na mwelekeo daima ni kujenga, Taifa kwanza tumeamua kuandaa ripoti hii ya uchambuziwa bajeti ili kutekeleza wajibu wetu. Kwa hiyo lengo la andiko hili ni kama ifuatavyo;

a) kuweka bayana uchambuzi mfupi wa mwenendo wa mapato na matumizi, na kushauri kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22
b) kupendekeza namna bora ya kuimarisha na kuongeza mapato ya serikali
c) kuangalia namna utekelezaji wa sera ya viwanda inavyochangia ukuaji wa uchumi na bajeti ya serikali
d) kuangalia namna TEHAMA na mifumo ya kielektroniki inavyoweza kuboreshwa kusaidia ukusanyaji na usimamizi wa mapato kwa njia bora zaidi.

Dhamira kubwa ni kuyafanya hayo yote kwa maslahi mapana ya taifa, kukuza uchumi ili mwisho wa siku maslahi ya wafanyakazi ambao ni nguzo muhimu yaweze kuboreshwa. Lengo la uchambuzi huu, ni kuangalia ni jinsi gani hivyo vyote vitakamilishwa kwa maslahi ya wadau wote wa bajeti ya taifa na wanufaike na bajeti hiyo wakati wa utekelezaji wake. Wadau hao ni wakulima, wafanyakazi, wafugaji, wafanyabiashara na wananchi wote kwa ujumla.

## 2. Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na Mipango ya Taifa ya Maendeleo Katika Kufikia Uchumi wa Kati

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ilianza kutekelezwa mwaka 2000 ili kuongoza harakati za maendeleo ya kiuchumi na kijamii zitakazoiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa kati na kuondokana na umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2025. Dira hii imeainisha malengo makuu matano ambayo ni: (i) Kuboresha hali ya maisha ya watanzania; (ii) Kuwepo kwa mazingira ya amani, usalama na umoja; (iii) Kujenga utawala bora; (iv) Kuwepo jamii iliyoelimika vyema na inayojifunza; na (v) Kujenga uchumi imara unaoweza kukabiliana na ushindani kutoka nchi nyingine.

Ili kutimiza malengo hayo, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali zikiwemo za kuandaa mipango na mikakati ya utekelezaji wa dira ya Taifa ya Maendeleo. Baadhi ya Mikakati na Mipango ya maendeleo iliyoanzishwa ni pamoja na *Mpango wa Maboresho ya Utumishi wa Umma, Malengo ya Maendeleo ya Millenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA), Mpango Elekezi wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka 15, Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16), Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2012/13, Mkakati wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021),* pamoja *na Mpango wa tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/2026).* Mipango yote hii inatekelezwa kwa kufuata Ilani ya Chama cha Mapinduzi inayoandaliwa kila baada ya miaka mitano.

Lengo la kuandaa mipango na mikakati yote ni kuhakikisha serikali inaendelea kuboresha viashiria muhimu vya uchumi, ikiwa ni pamoja na kuchochea ukuaji wa pato la taifa, kuimarisha sarafu/ shilingi ya nchi, kudhibiti mfumuko wa bei, kuimarisha Mazingira ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuvutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi, kuongeza ajira kwa wananchi hasa kundi la vijana pamoja na kufungamanisha sekta mbalimbali za kiuchumi na maendeleo ya watu.

Ili kuwezesha utekelezaji wa dira ya Taifa ya Maendeleo pamoja na utekelezaji wa Mipango na Mikakati ya maendeleo, THTU inashauri utekelezaji wa mambo yafuatayo;

a) serikali kupitia bajeti ya 2021/22 ihakikishe kwamba inaendelea kutoa kipaumbele kwenye sekta zinazofungamanisha uchumi wa viwanda na maedeleo ya watu katika kuboresha sekta za kijamii ikiwemo upatikanaji wa maji mijini na vijijini na kukiwezesha kilimo cha umwagiliaji; kuboresha huduma za afya katika hospitali zilizopo na zinazoendelea kujengwa ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa, madawa na kuongeza wataalamu wa afya; kuboresha vyanzo vya nishati endelevu ikiwemo umeme wa kutosha na wa uhakika pamoja na kuweka kipaumbele katika umeme wa nguvu za jua na upepo; kujenga na kuimarisha

miundombinu ya maghala yenye sifa ya kuhifadhi vyakula katika ubora unaostahili; kuweka muongozo mzuri wa aina ya viwanda vinavyoanzishwa na kuimarisha uwezo wa taasisi zetu za elimu na mafunzo (VET) ili kuandaa wataalamu na wabobezi wengi zaidi hasa katika nyanja zinazogusa sekta za kitaifa zinazotegemewa na kugusa watanzania wengi kama kilimo, ufugaji na uvuvi, ujasiriamali na biashara ndogo na za kati.

b) Serikali ihakikishe kwamba bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 inaendelea kuangazia mambo muhimu yaliyopo kwenye ilani kama vile: kuongeza kasi ya kupima maeneo ya wakulima, wafugaji na wavuvi pamoja na kuwapatia hati miliki za kimila ambazo watazitumia kama dhamana ya kuwawezesha kupata mikopo ya kuendeleza shughuli zao za kilimo, ufugaji, uvuvi na nyinginezo; kuongeza kasi ya kurasimisha biashara na kuwapatia wafanyabiashara wadogo maeneo ya kufanyia biashara, leseni na fursa za kupata mikopo yenye masharti nafuu; na kuboresha mfuko wa wanawake na vijana katika kuwapatia mikopo yenye riba nafuu isiyo na masharti magumu ili kuchochea fursa za ajira hasa zinazojielekeza katika sekta zenye kuhusisha makundi makubwa ya watanzania wanaotegemea ujasiriamali, kilimo, sanaa, michezo na burudani na sekta ya usafirishaji.

c) Kuhusu maboresho katika sekta ya umma, THTU inaishauri serikali kuhakikisha unakuwepo mfumo mzuri wa utumishi wa umma utakaochangia kujenga utawala bora unaosimamia vyema matumizi ya rasilimali za taifa kwa manufaa ya wote, ambao kwa namna nyingine utasaidia katika upatikanaji wa mapato zaidi yatakayotumika katika kuongeza kiwango cha stahiki za watumishi hivyo kuboresha hali ya maisha ya watu, kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

d) Kuhusu kudhibiti mfumko wa bei, serikali iendelee kuimarisha jitihada za kuangalia maeneo yanayosababisha mfumuko wa bei kama vile bei ya mafuta, sera za fedha na bidhaa nyingine muhimu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, kama vile chakula na madawa. Serikali ihakikishe vyakula na madawa yanayoweza kuzalishwa na kuongezwa thamani hapa nchini vizalishwe na kuimarisha uwepo wa kutosha katika soko la ndani. Udhibiti wa sera za fedha ni muhimu ili kutunza thamani ya fedha na kuchochea ukuaji wa uchumi kama vile kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za kigeni kwa huduma zinazotolewa ndani ya nchi.

e) Kuhusu kutetereka kwa uchumi wa dunia ulioporomoka kutoka asilimia 3.6 mwaka 2018 hadi 2.9 mwaka 2019 kutokana na janga la ugonjwa wa Korona (The COVID-19 pandemic) lililopelekea kufungwa kwa shughuli nyingi za kiuchumi ikiwemo utalii, safari za ndege na shughuli nyinginezo, na kuathiri sehemu kubwa ya uchumi wa dunia, kikanda na makusanyo ya mapato ya ndani, THTU inaishauri serikali kuendelea kuchukua hatua za kisera, kiutawala na

kiutendaji kurejesha biashara zilizoathirika moja kwa moja kutokana na janga la Corona pamoja na sekta tanzu zinazotegemea shughuli za kibiashara katika utekelezaji wake.

f) Kuhusu kuongezeka na kukua kwa deni la Taifa kufikia shilingi trilioni 59.01 sawa na asilimia 7.6 ya pato la taifa kutoka mwaka 2019 mpaka Desemba 2020 ambapo kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi trilioni 42.83 na deni la ndani ni shilingi trilioni 16.18. THTU inashauri kwamba, serikali iangalie uwezekano kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 kuweka utaratibu wa kulipa madeni ya ndani na nje; pamoja na, madeni ya wakandarasi wa ndani na malimbikizo ya stahiki mbalimbali za wafanyakazi wa umma. Inashauriwa kwamba ukopaji utakaofanyika kwa mwaka wa fedha 2021/22 uwe kwa ajili ya miradi ya maendeleo na inayoleta tija kwa taifa. Kwa nyongeza, utaratibu wa ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi (PPP) utumike kikamilifu ili baadhi ya gharama zibebwe na sekta binafsi kwa niaba ya serikali.

g) Kuboresha mazingira ya utulivu wa kisiasa na kijamii. Ni muhimu kuzingatia mambo makuu manne aliyotuachia Baba wa taifa Mwalimu Nyerere (Ardhi, watu, uongozi bora na siasa safi). Msisitizo zaidi uwe kwenye uongozi bora na siasa safi kwani mawili yaliyobaki hutegemea haya mengine.

## 3. Sera, Mwenendo na Tathmini ya Bajeti


Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2016/17 – 2020/21) serikali imefanya juhudi katika kutafuta mbinu mbadala za kuongeza na kuimarisha mazingira ya kukusanya pato la ndani. Juhudi hizi zinajumuisha kufanya marejeo ya baadhi ya sheria za kodi ili ziweze kuendana na mazingira ya nchi yaliyopo. Malengo makuu ya kisera katika kuongeza makusanyo ya mapato ni pamoja na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija, kuongeza utumiaji wa mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato, kuendelea kuboresha usimamizi na ukaguzi kwenye mipaka ya nchi, bandari na viwanja vya ndege, na kupanua wigo wa mapato. Sanjari na hilo, serikali imekua ikiweka vipaumbele katika kuongeza ufanisi wa matumizi ya mapato, miongoni mwa vipaumbele hivyo ni pamoja na kudhibiti ongezeko la malimbikizo ya stahiki za wafanyakazi pamoja na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Ufanisi wa makusanyo upande wa Serikali za Mitaa umekua duni, kwa mfano kwa wastani wa kipindi cha miaka mitatu iliyopita ni asilimia 79 tu ya makusanyo yalipatikana ikilinganishwa na lengo lililowekwa. Juhudi kwenye kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato, urasimishaji wa sekta zisizo rasmi, kuimarisha taasisi husika na kuwezesha mazingira rafiki ya uwekezaji na uanzishwaji wa viwanda na kuongeza wigo na usimamizi wa makusanyo yatokanayo na kodi za mifugo, nyumba, ardhi na maliasili nyingine kama misitu, madini, utalii, gesi asilia na samaki bado unahitajika.

Malipo ya mishahara ya wafanyakazi yamekuwa hayafikii malengo kwa kipindi cha miaka mitano. Kutofikia lengo la bajeti eneo hili kunaibua malimbikizo mapya yanayoongeza deni la serikali la ndani na kupelekea jumla ya deni la nchi kufikia asilimia 7.6% kwa mwaka 2021/22.

Katika mwaka 2021/22, Serikali imepanga kutumia jumlaya shilingi trilioni 36.26 kwa matumizi ya kawaida namaendeleo. THTU inashauri Serikali iendelee kutekeleza hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyajiwa mapato ya ndani ilikupunguza utegemezi, kugharamia mahitaji yasiyo epukika kama vile ugharamiaji wa miradi ya kipaumbele na kimkakati, denial Serikali, mishahara ya watumishi na kuwapandisha vyeo kwa wakati ili kuongeza morali ya watumishi wa umma. Takwimu za miaka minne mfululizo zinaonyesha kuwa bajeti ya mishahara haiendani na uhalisia wa malipo ya mishahara kama Kielelezo Na. 1kinavyofafanua zaidi.

**Kielelezo Na.  1 : Uhusiano wa Bajeti na Malipo Halisi ya Mishahara**




**Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango**

THTU inaamini na kutambua vigezo vilivyo tumika katika uandaaji wa kiwangocha ukomo wa bajeti za matumizi za Mafungu ni pamoja na:miradi inayoendelea; matumizi yaliyolindwa; vibalivya miradi mipya; miradiyenye vyanzo maalumu; vibali vya ajira mpya na upandishwajiwa madaraja kwa watumishi; matumizi yasiyojirudia; na mahitaji ya Mamlaka za Uhifadhi zilizo athiriwa na kushuka kwa biashara katika sekta ya utalii.

## 4. Uboreshaji wa Mifumo ya Ukusanyaji Kodi katika Kuongeza Uwezo wa Serikali Kimapato

Eneo la mifumo inayosaidia kuongeza ufanisi wa kukusanya mapato ya aina tofauti ya serikali limeonekana linakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo kutokuwepo kwa mifumo thabiti yenye ufanisi kwenye ngazi zote. Pamoja na juhudi za sasa za ukusanyaji na usimamizi wa mapato, bado uboreshaji unapaswa kuendelezwa kutokana na changamoto za makuzi ya kiteknolojia. Matumizi mazuri ya TEHAMA na mifumo ya kielektroniki ya kumtambua mlipa kodi na kukusanya mapato limeonekana ni jambo muhimu. Yafuatayo ni mapendekezo ya kimkakati juu ya uboreshaji na uimarishaji wa mifumo ya kielektroniki ya mapato, ambayo hatimaye yatasaidia katika ukusanyaji wa mapato kwa njia bora zaidi kuliko ilivyo sasa:

a) Uboreshaji wa mbinu za ulinzi wa mifumo ya huduma mbalimbali zinazohusiana na ukusanyaji wa kodi ili kupambana na uhalifu wa kimtandao unaoweza kuathiri ukusanyaji na upatikanaji wa taarifa sahihi za mapato. Ripoti ya National Cyber Security Index (NCSI) ya mwaka 2021 imeiorodhesha Tanzania kwenye nafasi ya 130 kidunia na ya nne kwa ukanda wa Afrika Mashariki kwa usalama wa mtandao. Pamoja na uwepo wa sheria ya udhibiti wa makossa ya mtandao, bado takwimu zinabainisha Tanzania ni miongoni mwa nchi zisizo na usalama wa kuridhisha kimtandao. Aidha, ripoti ya NCSI, inabainisha kuwa Tanzania inapaswa kuongeza ufanisi katika utengenezaji wa sera za ulinzi wa mtandao, kuongeza uwezo wa uchakataji wa taarifa za viashiria vya uhalifu wa mtandao, elimu ya usalama wa mtandao, ushirikiano kimataifa katika kupambana na uhalifu wa mtandao, ulinzi wa huduma za mtandao, utambuzi wa kielektroni (e-identity), usalama wa data za watumiaji wa huduma za kielektroniki (data protection) na uboreshaji wa ulinzi wa mtandao dhidi ya udukuzi wa mifumo ya serikali hususani ya mapato. Tunapendekeza uwekezaji katika tafiti na nguvu kazi katika kuongeza usalama wa mtandao.

b) Kuboresha mfumo tangamani wa matumizi (framework of adoption) ya TEHAMA katika serikali ili kuwa na ufanisi wa kuiboresha, kuikagua na kuunganisha. Uboreshaji huo utasaidia kupunguza hatari za uvamizi wa kimtandao na udukuzi. Kwa hali ya sasa mifumo mingi haijaunganishwa kufanya kazi pamoja na mifumo mingine ya serikali kutokana na makusudio ya uundwaji wake na miundo yake kiteknolojia. Hii ni changamoto inayokabili mifumo mingi ya kielektroniki ya huduma (e-sevices) kutokana na ukosekanaji wa viwango vya kitaifa na kimataifa, mfano namba msimbo za huduma (service codes).

c) Ukosekanaji wa mahusiano kati ya mifumo mbalimbali, mbali na kuongeza gharama za utendaji wake pia unaathiri tija ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa taarifa sahihi za mifumo tofauti inayoingiliana. Kupitia wakala wa serikali

mtandao na taasisi za tafiti, juhudi za pamoja ziongezwe katika kutengeneza na kuhuisha kanuni na viwango vya ubora wa mifumo ya TEHAMA inayotumika serikalini.

d) Pamoja na uimarishwaji wa sera na miongozo mbalimbali yenye kulinda usalama wa mifumo ya TEHAMA, tunapendekeza juhudi zaidi zielekezwe katika kujenga uwezo wa ndani katika kuunda na kuratibu mifumo ya serikali hasa inayohusiana na mapato. Hii itaimarisha uzalendo na usalama wa nyaraka za mapato, vile vile itapunguza gharama kubwa zinazolipwa na serikali kwa makampuni ya kigeni katika kununua mifumo ya TEHAMA na ushauri wa kitaalamu. Mifumo yenye maslahi mapana ya nchi mfano, mfumo wa manunuzi serikalini, mfumo wa ulipaji n.k, itengenezwe na wazawa na kuhodhiwa ndani ya nchi ili kulinda maslahi ya nchi.

e) Kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mifumo ya TEHAMA inayohusiana na ukusanyaji na usimamizi wa kodi. Hii itasaidia uhakiki wa mapema wa ubora wa mifumo hiyo na kuibua mianya ya udukuzi na udanganyifu inayoweza kutokea kutokana na ukuaji wa teknolojia. Hali kadhalika, mapitio ya mara kwa mara yatasaidia mifumo hiyo kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia. Sambamba na hayo, tunapendekeza uhuishwaji wa sheria na kanuni ya serikali mtandao katika taasisi za umma ili kuimarisha utangamano wa uratibu wa serikali mtandao kufikia malengo tarajali.

f) Kuweka mikakati ya kuboresha kanzidata ya huduma, bidhaa sambamba na taarifa za walipa kodi. Mfano taarifa za majengo, ununuzi na umiliki wa ardhi, matangazo ya biashara, leseni mbalimbali n.k. Mikakati hii iende sambamba na kurasimisha namba msimbo (service codes) za huduma mbalimbali ili kuwezesha ubadililishanaji wa taarifa (data sharing) kati ya mifumo mbalimbali ya huduma ili kuongeza ufanisi. Aidha uunganishwaji wa mifumo hii utawezesha upatikanaji wa takwimu sahihi kwa wakati na kuweza kutumiwa na wadau tofauti ili kurahisisha ufuatiliaji, utambuzi na utoaji wa msaada hasa kwa walengwa kwenye jamii, biashara, uwekezaji, viwanda n.k.

g) Katika kuongeza usimamizi na ufuatiliaji wa vyanzo vya mapato, matumizi madhubuti ya TEHAMA katika kutengeneza ramani za kidigitali zitakazosaidia serikali kuimarisha viwango vya ukusanyaji mapato na kutoa maelezo ya biashara zote na majengo ambayo yanapaswa kulipiwa ada mbalimbali ikiwemo ile ya ardhi. Kwa ujumla wake matumizi haya ya teknolojia hususani TEHAMA mamboleo yatawezesha takwimu kupatikana kwa urahisi na hivyo kurahisisha kuongeza ufanisi wa mipango mikakati ya maendeleo.

h) Mamlaka ya kodi na taasisi nyingine za serikali zinazohusika na ukusanyaji wa tozo na ada mbalimbali zinapaswa kuhakikisha mchakato wa malipo unakuwa rafiki kuanzia usajili hadi malipo. Aidha, mifumo ya kodi inapaswa kuwa rafiki kwa namna ambayo itaruhusu walipa kodi kujikadiria (self assessment) ikiwa ni

pamoja na upatikanaji wa taarifa zao za kodi. Kwa mfano, taarifa kwa wadau kuhusu ukomo wa tozo, ada, kodi n.k. Taarifa hizo zinaweza kupatikana muda wowote au kutumwa kwa mhusika kwa njia ya ujumbe mfupi, kwa mfano wiki mbili kabla ya ukomo wa uhalali wa malipo hayo kufikia.

i) Tunapendekeza uwekezaji katika ubunifu wa mifumo ya TEHAMA mamboleo hususani "Blockchain" na "Artificial Intellegence" katika kuimairisha umadhubuti wa intelijensia ya usalama na ufanisi wa mifumo ya kodi. Teknolojia hizi zimetumika katika nchi mbali mbali kama Afrika Kusini na Senegal kwa mafanikio makubwa, hivyo ni muhimu mamlaka ya usimamizi wa kodi (TRA) kuamua pia kutumia mifumo hiyo.

## 5. Mapendekezo ya THTU juu ya namna bora ya kutekeleza sera ya viwanda na namna itakavyosaidia kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

Kama ambavyo kauli mbiu ya THTU inaeleza kuwa "**Nia na Mwelekeo wetu Daima niKujenga, Taifa Kwanza**", katika kuendelea kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu tunashauri yafuatayo:

a) Serikali ielekeze nguvu katika kuchochea viwanda vinavyotumia malighafi nyingi za ndani zinazotokana na mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Hii itachochea uzalishaji wa ndani, kukuza kipato cha wazalishaji wa malighafi hizo na kukuza pato la taifa.

b) Ushirikishwaji wa wadau mbalimbali (wawekezaji, sekta za umeme na maji, usafirishaji n.k) katika maamuzi na uandaaji wa miongozo mbalimbali inayohusiana na sera ya viwanda. Hii itasaidia kuwa na dhamira ya pamoja katika utekelezaji wa sera ya viwanda.

c) Kuimarisha sekta za kilimo, uvuvi na ufugaji. Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 ielekeze nguvu katika kuimarisha miundombinu na masoko ya mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji. Hii itachochea upatikanaji wa malighafi nyingi muhimu kwa viwanda.

d) Kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya kimkakati na kuimarisha vilivyopo ili kuongeza thamani ya bidhaa za mazao hayo kwa mfano korosho, chai, pamba, kahawa, alizeti, matunda na mbogamboga ambayo pia itasaidia kukuza ajira na kuongeza ukusanyaji wa mapato.

e) Kuvijengea uwezo zaidi vituo na vyuo vya ufundi stadi vya juu, kati na vidogo ili kuwasaidia vijana kuweza kujiajiri wenyewe kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vitakavyochochea ukuaji wa pato la taifa.

f) Kuongeza kasi ya uimarishaji wa masoko na miundombinu hasa ya barabara vijijini ili kuchochea biashara, uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya kilimo; sekta

ambayo inategemewa na asilimia kubwa ya watanzania waishio vijijini na pia viwanda vingi vidogo, vya kati na vikubwa kama chanzo cha malighafi.

g) Serikali iendelee kuweka sera rafiki na wezeshi kwa wawekezaji wa viwanda katika upatikanaji wa nishati na malighafi ili kupunguza gharama za uzalishaji. Hii itawasaidia wafanyakazi nchini na wananchi kwa ujumla kuweza kumudu gharama za manunuzi (increase of purchasing power) kwa kuwa bidhaa zitauzwa kwa bei nafuu hivyo kupungua kwa gharama au ukali wa maisha kwa wafanyakazi nchini.

h) Serikali iendelee kuimarisha mifumo ya ukusanyaji kodi, na kuimarisha mifumo ya kutoa misamaha na unafuu wa kodi kwa wawekezaji. Mifumo ya ukadiriaji na utozaji kodi ikiwa rafiki itasaidia ulipaji kodi kwa hiari (voluntary tax compliance) na kuimarisha ukusanyaji mapato.

i) Tunasisitiza serikali iendelee kusimamia sera ya ajira za kwenye viwanda na kuimarisha vipengele vya mikataba ya wawekezaji vinavyowabana kutoa nafasi nyingi za ajira kwa watanzania.

j) Serikali iendelee kuimarisha viwanda vikubwa vya uzalishaji (manufacturing industries) ili vifaa vinavyotumika katika miradi mikubwa ya ujenzi vizalishwe na kupatikana nchini.

## 6. Maoni katika kuboresha bajeti ya Serikali

Ili kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, sera za mapato kwa mwaka wa fedha 2021/22 zijikite katika kuongeza na kuboresha vitu vifuatavyo:

### 6.1. Kuongeza wigo wa kodi

Maeneno muhimu ambayo tunaishauri serikali izidi kuangazia katika kuongeza mapato (kuwepo na mbinu bunifu, rafiki, shirikishi na za kimkakati), kama ifuatavyo: -

a) Kuendelea kurasimisha sekta zisizo rasmi na kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kupata vyanzo vipya vya mapato, mfano uthaminishaji wa majengo na kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi, kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo wadogo kama Machinga, wavuvi, shughuli za ufundi na mama lishe. Mfumo wa kielektroniki utasaidia kuwatambua na kutengeneza mfumo rafiki wa kuwatoza kodi.

b) Michezo ya kamari na michezo ya kubahatisha kuongezewa kiwango cha kodi kwa mfano kutoka asilimia 18 hadi 30 (serikali ya Kenya wao wanatoza asilimia 35 ya pato ghafi) hii itasaidia pia kuondoa uraibu kwa vijana na kuelekeza nguvu kwenye shughuli zingine za kimaendeleo.

c) Misamaha ya kodi itathiminiwe, isiyo na tija ipunguzwe zaidi ili kuongeza makusanyo ya serikali. THTU inatambua umuhimu wa misamaha ya kodi katika

kuchochea maendeleo hasa maendeleo jamii na uwekezaji. Hii ni kutokana na ukweli kwamba ipo baadhi ya misamaha ya kodi inayotolewa hutumika isivyotakiwa kinyume na malengo ya utolewaji wake, kwani baadhi ya watu hutumia vibaya misamaha hiyo kujinufaisha binafsi na kuipotezea serikali mapato. THTU inashauri kuwepo umakini katika ufuatiliaji wa kina kwenye misamaha hiyo ili itumike kama ilivyokusudiwa. Kwa mujibu wa ripoti za mapato ya kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na hotuba ya bajeti ya Waziri wa Fedha iliyosomwa Bungeni wakati wa uwasilishaji wa bajeti ya serikali kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, Tanzania imeonekana ni miongoni mwa nchi zenye misamaha mingi ya kodi katika Ukanda wa Afrika Mashariki.

d) Kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi: Sheria yetu ya kodi ya mapato (Income Tax Act) na sheria nyingine za kodi ziendelee kuboreshwa ili kusaidia kupunguza mianya ya ukwepaji kodi kwa sheria hizo (Tax avoidance). Pia tunashauri serikali izidi kuboresha mifumo ya ukusanyaji kodi na hasa kutumia teknolojia za kielektroniki kupunguza wakwepa kodi ambao mamlaka ya mapato (TRA) inashindwa kuwafikia au kupata taarifa zao kwa usahihi na kuwezesha kukwepa kodi na kuipunguzia mapato serikali. Mfano, watoa huduma hasa wa elimu katika sekta binafsi kwenye ngazi zote wanaweza kutozwa kodi kwenye bidhaa wanazoweza kuzinunua kwenye soko huria.

e) Kuongeza ufanisi na juhudi katika elimu ya mlipa kodi: Hii itaongeza uelewa wa kodi kwa wananchi na motisha ya walipa kodi kupenda kulipa kodi bila shuruti (Voluntary Tax Compliance). Matumizi ya TEHAMA yanaweza kusaidia kueneza elimu ya mlipa kodi kwa haraka kuliko ilivyo sasa. Mamlaka husika zijikite katika kubuni mifumo rahisi ya kufikisha elimu hii kwa walipa kodi kupitia simu za mkononi na mitandao ya kijamii.

f) Tunashauri Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ichukue hatua za makusudi za kuboresha mahusiano kati yake na walipa kodi (to increase voluntarily tax compliance) kwa lengo la kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwa walipa kodi kuwa TRA inatumia nguvu na vitisho kudai kodi na hivyo kuzorotesha ukusanyaji wa mapato. Kwa mfano badala ya maafisa wa TRA kufunga biashara za wananchi wanaweza kutumia njia mbadala za kulipa kodi kwa awamu (installments) kwa muda maalum utakaokubalika na mamlaka ya mapato Tanzania (TRA).

g) Tunapendekeza kuboresha Mfumo Mpya wa stampu za Kodi za kielektroniki kwa bidhaa zote nchini. Mfumo mpya wa stampu za Kodi za kielektroniki utaiwezesha Serikali kutumia teknolojia ya kisasa kupata taarifa sahihi za uzalishaji viwandani na kwa wakati (real time) zinazotumika kupanga mipango ya maendeleo ya Taifa. Pia mfumo huu mpya utaiwezesha Serikali kudhibiti uvujaji wa mapato na kutambua mapema kiasi cha Kodi ya Ushuru wa Bidhaa, Kodi ya Mapato na ile ya Ongezeko la Thamani (VAT) itakayolipwa. Aidha, mfumo wa stampu za Kodi

za kielektroniki utadhibiti tatizo la uwepo wa stempu za karatasi za kughushi linalochangia uwepo wa bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora na zinazoweza kuathiri afya za binadamu. Mfumo huu mpya unatumika katika nchi nyingine ikiwa pamoja na Kenya, Morocco, Uturuki, Malaysia, Afrika Kusini Pamoja na Uswisi ambao umekuwa na mafanikio makubwa. Pia kutiliwe mkazo kwenye stampu za mikataba ambapo uzoefu unaonyesha mikataba mingi haiwekwi wazi ili stamp zitakazowekwa ziakisi thamani halisi ya mkataba.

### 6.2. Kupunguza changamoto zinazohusiana na mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Kupungua kwa changamoto hizi kutachangia kukuza biashara zilizopo (kukuza mitaji) na pia kukaribisha wawekezaji wapya na kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya serikali. Baadhi ya changamoto ambazo zinapaswa kumulikwa zaidi ni hizi zifuatazo:

a) Migongano ya sheria, kanuni na taratibu zinazotumiwa na mamlaka mbalimbali;
b) Gharama kubwa za kuanzisha na kuendesha biashara kutokana na wingi wa kodi, ada na tozo zinazoambatana na taratibu ngumu na nyingi zenye urasimu usio na tija na hivyo kutoa mianya na mazingira ya rushwa; na,
c) Muingiliano wa majukumu na wingi wa mamlaka za udhibiti katika kuidhinisha na kutoa hati, vibali na vyeti kwenye shughuli za uwekezaji na biashara.

### 6.3. Usimamizi na ukaguzi kwenye kampuni ambazo Serikali ina hisa

Ofisi ya Msajili wa Hazina iimarishe usimamizi na ukaguzi kwenye kampuni ambazo Serikali ina hisa ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata gawio stahiki katika uwekezaji wake.

### 6.4. Miradi ya Serikali za Mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa zijielekeze kwenye miradi itakayochochea upatikanaji wa mapato katika mamlaka hizo hususani viwanda, masoko, machinjio ya kisasa, stendi za mabasi, stendi za maegesho ya malori, ushuru wa mazao na maghala ya kuhifadhi nafaka. Ili kupunguza utegemezi wa serikali kuu tunashauri:

a) Maafisa Masuuli wazidi kusisitizwa kutumia wakandarasi na watoa huduma wanaotumia mashine za kielektroniki za kukusanya mapato na ambao wanarekodi safi za kulipa kodi kutoka mamlaka ya mapato (TRA);
b) Kuongeza wigo wa kodi hasa kwenye elimu huria ambapo watoa huduma wengi sio rasmi na wanafanya biashara kinyemela bila kuwajibika kwenye mmlaka husika za ukusanyaji mapato.

c) Pia tunapendekeza sheria ya madini iangaliwe vizuri ili kodi stahiki ya serikali iweze kukusanywa.

## 7. Mapendekezo juu ya Kodi ya Mapato ya Ajira (PAYE)

Tunachukua fursa hii kuipongeza serikali kwa kuboresha jedwali la kodi (Tax Bracket) kwenye kodi ya kipato cha ajira ambapo kimesogeza kima cha chini kutoka 170,000 hadi 270,000. Kupitia mabadiliko haya wafanyakazi wamenufaika kwa kiasi kutokana na nafuu ya kodi (Tax relief).

**Jedwali Na. 1: Utozaji kodi kabla ya mwaka wa fedha 2020/2021**

| **Kodi ya Mapato ya mtu binafsi (Tanzania Bara) – Iliyokuwepo** | |
|---|---|
| **Mapato kwa Mwezi** | **Kiwango cha Kodi** |
| Mapato yasiyozidi Sh.170,000 | Hakuna Kodi |
| Mapato yanayozidi Sh.170,000 lakini hayazidi Sh. 360,000 | 9% ya mapato yanayozidi sh. 170,000 |
| Mapato yanayozidi Sh. 360,000 lakini hayazidi Sh. 540,000 | Sh.17,100 + 20% ya mapato yanayozidi Sh.360,000 |
| Mapato yanayozidi Sh. 540,000 lakini hayazidi Sh. 720,000 | Sh.53,100 + 25% ya mapato yanayozidi Sh. 540,000 |
| Mapato yanayozidi Sh.720,000 | Sh.98,100 + 30% ya mapato yanayozidi Sh. 720,000 |

**Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango**

**Jedwali Na. 2: Utozaji kodi kwasasa**

| **Mapato kwa Mwezi** | **Kiwango cha Kodi** |
|---|---|
| Mapato yasiyozidi 270,000/= | Hakuna Kodi |
| Mapato yanayozidi 270,000/= lakini yasiyozidi Tshs. 520,000/= | 9% ya mapato kinachozidi Tshs. 270,000/= |
| Mapato yanayozidi 520,000/=lakini yasiyozidi 760,000/= | Tshs. 22,500/= + 20% ya mapato yanayozidi 520,000/= |
| Mapato yanayozidi 760,000/=lakini yasiyozidi 1,000,000/= | Tshs. 70,500/= + 25% ya mapato yanayozidi 760,000/= |
| Mapato yanayozidi 1,000,000/= | Tshs. 130,500/= + 30% ya mapato yanayozidi 1,000,000/= |
| **Zingatia:Kima cha chini: kipato kwa mwaka kisichozidi Ths 3,240,000/= hakuna kodi** | |

**Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango**

Aidha, pamoja na kuipongeza serikali kwa kazi nzuri iliyofanya na kuchukua hatua kwenye mabadiliko ya jedwali la kodi ya kipato. Bado tunaiomba serikali iendelee kuboresha jedwali la kodi ili kumpatia nafuu zaidi mfanyakazi kwa kuongeza kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 270,000 kilichopo sasa hadi kufikia shilingi 360,000; Jedwali namba 3 linafafanua kwa kina mapendekezo yetu kuhusiana na kodi ya kipato cha ajira. Mapendekezo haya yamezingatia mifumo ya kodi ya nchi nyingine za Afrika Mashariki na za kusini mwa jangwa la sahara kulingana na ukuaji wa uchumi wa nchi, pia kukabiliana na mfumuko wa bei.

**Jedwali Na. 3: Mapendekezo ya utozaji kodi baada ya Mabadiliko**

| **Kodi ya Mapato ya mtu binafsi (Tanzania Bara) – Tunayopendekeza** | |
|---|---|
| **Mapato kwa Mwezi** | **Kiwango cha Kodi** |
| Mapato yasiyozidi Sh.360,000 | Hakuna Kodi |
| Mapato yanayozidi Sh.360,000 lakini hayazidi Sh. 540,000 | 9% ya mapato yanayozidi sh. 360,000 |
| Mapato yanayozidi Sh. 540,000 lakini hayazidi Sh. 780,000 | Sh.27,900+ 20% ya mapato yanayozidi Sh.540,000 |
| Mapato yanayozidi Sh. 780,000 lakini hayazidi Sh. 1,020,000 | Sh.118,500 + 25% ya mapato yanayozidi Sh. 780,000 |
| Mapato yanayozidi Sh.1,020,000 | Sh.228,375 + 30% ya mapato yanayozidi Sh. 1,020,000 |

**Chanzo: Maoni ya THTU 2021/2022**

## 8. Mapendekezo ya mabadiliko ya ada na tozo mbali mbali.

Katika kupanua wigo wa ukusanyaji mapato ya serikali na kuwezesha serikali kuweza kuhudumia zaidi wananchi wake, tunashauri mabadiliko yafuatayo kwenye tozo na ada mbali mbali.

**Jedwali Na. 4: Ada za huduma ya Bandari**

| **Chanzo cha kodi** | **Iliyopo** | **Inayopendekezwa** | **Badiliko** |
|---|---|---|---|
| Kwa wasafiri wakazi | TZS 500 | TZS 700 | 40% |
| Kwa wageni | $ 5 | $ 7 | 40% |

**Jedwali Na. 5 : Ada za Michezo ya kubahatisha**

| **Chanzo cha kodi** | **Iliyopo** | **Inayopendekezwa** | **Badiliko** |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| Casino ya Ardhini | 18% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi | 25% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi | 7% |
| Casino ya Mitandaoni | 25% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi | 30% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi | 5% |
| Kodi kwenye ushindi | 20% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi | 30% ya mapato baada ya kuondoa gharama za washindi | 10% |
| Kodi kwenye ushindi kwenye Casino | 12% kwa mapato ya Casino | 15% kwa mapato ya Casino | 3% |

## 9. Mfanyakazi na mfumuko wa bei.

Mfumuko wa bei ni suala muhimu sana kwa mfanyakazi na wananchi wengine kwani lina athari kwenye kipato na nguvu ya manunuzi. THTU inaipongeza serikali kwa kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei wa bidhaa na huduma, lakini inashauri serikali kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei ili kipato cha mfanyakazi kiwe na tija.

Kwa kipindi cha mwaka ulioisha mfumuko wa bei upo kwenye tarakimu moja na udhibiti wake umeendeleakama inavyoainishwa hapa chini kutoka kwenye ofisi ya taifa ya takwimu.

**Jedwali Na. 6: Mfumuko wa bei**


| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Oktoba, 2019 | Septemba, 2020 | Oktoba, 2020 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi. | 38.5 | 119.30 | 123.27 | 123.33 | 0.0 | 3.4 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku. | 3.7 | 110.63 | 109.93 | 109.93 | 0.0 | -0.6 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu. | 8.3 | 112.39 | 114.75 | 114.63 | -0.1 | 2.0 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4 | Nishati, Maji na Makazi. | 11.6 | 139.28 | 151.62 | 150.65 | -0.6 | 8.2 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba. | 6.3 | 112.07 | 113.84 | 113.78 | -0.1 | 1.5 |
| 6 | Gharama za Afya. | 2.9 | 109.55 | 110.49 | 110.50 | 0.0 | 0.9 |
| 7 | Usafirishaji. | 12.5 | 105.29 | 107.44 | 107.41 | 0.0 | 2.0 |
| 8 | Mawasiliano. | 5.6 | 96.26 | 96.67 | 96.65 | 0.0 | 0.4 |
| 9 | Utamaduni na Burudani. | 1.6 | 104.04 | 104.70 | 104.71 | 0.0 | 0.6 |
| 10 | Elimu. | 1.5 | 107.68 | 109.03 | 109.03 | 0.0 | 1.3 |
| 11 | Hoteli na Migahawa. | 4.2 | 110.63 | 112.44 | 112.44 | 0.0 | 1.6 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo. | 3.1 | 109.46 | 110.39 | 110.40 | 0.0 | 0.9 |
| **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | | **100.00** | **115.84** | **119.54** | **119.43** | **-0.1** | **3.1** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa nyumbani na migahawani. | 37.1 | 122.92 | 128.33 | 128.38 | 0.0 | 4.4 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika nyumbani pamoja na petroli na dizeli. | 8.7 | 150.96 | 160.80 | 159.57 | -0.8 | 5.7 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula. | 62.9 | 114.64 | 118.32 | 118.11 | -0.2 | 3.0 |
| 4 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, nishati na mafuta. | 54.3 | 108.82 | 111.52 | 111.48 | 0.0 | 2.4 |

***Chanzo: ofisi ya taifa ya Takwimu 2020.***

Kielelezo Na 2 kinaonesha kuwa fahirisi (index) za bei zimekuwa na mwenendo imara kutoka mwezi Oktoba, 2019 hadi mwezi Oktoba, 2020. Katika kipindi hicho, Mfumuko wa Bei ulikuwa kati ya asilimia 3.1 kwa mwezi Septemba na Oktoba, 2020 na asilimia 3.8 kwa mwezi Novemba na Desemba 2020. Pamoja na jambo hili zuri bado tunaamini serikali ikiboresha zaidi maslahi ya wafanyakazi, wataishi kwa uhakika wa kipato chao na kukabiliana na mfumuko wa bei ambao kimsingi huwa ni tishio kwao kwa kulinganisha kati ya kipato na uhalisi wa bei ambazo zipo sokoni.

**Kielelezo Na. 2: Farihisi za Bei**





**Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu**

## 10. Maoni ya THTU juu ya nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi na ajira mpya

Tunatambua juhudi kubwa zinazofanywa na serikali katika kuboresha maisha ya watanzania wakiwemo wafanyakazi wa umma na kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji kazi sekta bianfsi. Kazi kubwa imefanywa kwenye kuboresha miundombinu nakwa lengo la kuchochea mazingira ya uwekezaji na biashara. Pamoja na hayo bado, tunaiomba serikali ione umuihmu wa kuongeza mishahara kwa wafanyakazi kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022 ili kuboresha zaidi maslahi yao na kuwapatia motisha zaidi kwenye kulitumikia taifa.

Kwa mujibu wa wizara ya fedha, katika mwaka 2021/22, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 36.26 sawa na ongezeko la asilimia 4.0 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/21 ya shilingi trilioni 34.88. Katika kuhakikisha nchi inakuwa na uwezo wa kujitegemea serikali imeainisha lengo la kukusanya mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) shilingi trilioni 26.03 mwaka 2021/22 kutoka makadirio ya shilingi trilioni 24.07 mwaka 2020/21. KielelezoNa.3 linafafanua zaidi.

**Kielelezo Na. 3 Makadirio ya Mapato ya Ndani**





**Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango (2021)**

Kwa Muktadha huu, tunaishauri serikali kufikiria nyongeza ya mishahara ya mwaka (Annual Increments) kwa wafanyakazi ili kuboresha zaidi maisha yao kama ambavyo serikali imeendelea kuonyesha kusisitiza wakati wote juu ya suala hili.

Juhudi kubwa imefanywa na kuzingatia ushauri kwenye jedwali la kodi za mapato kwa wafanyakazi (PAYE – Tax Brackets) ambapo mabadiliko yamewanufaisha wafanyakazi kwenye unafuu wa kodi, lakini bado ni ombi la wafanyakazi kwamba serikali ipange naitenge bajeti kwaajili ya nyongeza ya mishahara ili kuendana na uhalisia wa hali ya maisha na mfumuko wa bei. Kielelezo Na. 4 kinaonyesha makisio ya matumizi ya serikali kwa kipindi cha miaka minne kuanzia 2020/2021 hadi 2023/2024.

**Kielelezo Na.  2 : Makisio ya Matumizi**




THTU ina imani na serikali katika mapendekezo ya makadirio ya matumizi (kama inavyofafanuliwa katika Kielelezo Namba 4) itaendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi na kuwapatia motisha zaidi.

## 11. Umuhimu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kuboresho Makusanyo Mapato na Matumizi

Maeneo muhimu ambayo serikali inashauriwa izidi kuangazia katika kuongeza mapato (uwepo wa mbinu bunifu, rafiki, shirikishi na za kimkakati), kama ifuatavyo: -

a) Kujenga mazingira wezeshi ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA kama nyezo ya kufungua fursa za uchumi wa kidigitali na mapinduzi ya nne ya viwanda kama chachu ya mapato ya ndani na nje. Katika kuliangazia suala hili THTU inapendekeza yafuatayo: -

   1) Kuondoa vikwazo katika matumizi ya TEHAMA katika kuwezesha ufanisi katika kufanya biashara. Maboresho yafanyike katika kupunguza tozo za usajili na uendeshaji wa miundombinu ya TEHAMA yenye tija ya kuzalisha fursa mpya za ajira. Mfano, kuondolewa kwa ada za usajili kwa wazalishaji wa maudhui na gharama za huduma ya mtandao wa mawasiliano (internet). Kwa upande wa wazalishaji wa maudhui mtandaoni tozo zifanyike kulingana na mapato wanayoyapata.
   2) Kutengeneza uwezo wa ndani wa kuzalisha vifaa vya TEHAMA ili kutengeneza ajira mpya, kuimarisha usalama wa mawasiliano na ubora wa vifaa vya TEHAMA vinavyotumiwa nchini. Katika hili tunaishauri serikali kupitia Wizara husika kuviwezesha vyuo vya kati, pamoja na tume ya sayansi

katika kufikia lengo hili. Sambamba na hili, THTU inaishauri serikali iwekeze katika kujenga uwezo wa uchakataji wa taka za kieletroniki ili kulinda mazingira ya asili.

3) Kuongeza kasi ya utekelezaji wa anuani za makazi na postikadi katika mikoa na majiji yote ili kuchochea fursa za kibiashara katika majukwaa ya kieletroniki.
4) Kuongeza uwekezaji katika tafiti za serikali mtandao na matumizi ya TEHAMA katika biashara ili kuibua fursa za kuboresha ufanisi zaidi kuliko ilivyo sasa.
5) Kudhibiti uhalifu wa kimtandao ili kuchochea imani na uthabiti wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA kwa wadau mbalimbali kuwekeza katika fursa zitokanazo na utandawazi.
6) Tunapendekeza uwepo wa utaratibu maalumu wa kisera wa punguzo la kodi kwa vifaa wezeshi vya miundombinu ya TEHAMA kwa taasisi za umma na makampuni yanayochipukia. Hii itaongeza motisha na kuchochea kasi katika matumizi ya TEHAMA yenye viwango kuelekea uchumi wa kidigitali na mapinduzi ya nne ya viwanda.
7) Tunapendekeza kuongeza matumizi ya TEHAMA mamboleo katika kukusanya na kuchakata data ili kuongeza intelijensia ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato kwa ufanisi zaidi.
8) Tunapendekeza kuboresha mazingira ya kuvutia wawekazaji hasa makampuni makubwa ya TEHAMA kuja kuwekeza nchini. Hii itachagiza ajira mpya, ukuaji wa kodi ya mapato na pia ukuaji wa matumizi ya tekenolojia katika nyanja mbalimbali za uchumi.

b) Kupunguza changamoto zinazohusiana na mazingira ya kufanyia biashara na uwekezaji nchini. Kupungua kwa changamoto hizi kutachangia kukuza biashara zilizopo (kukuza mitaji) na pia kuvutia wawekezaji wapya na kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya serikali. Baadhi ya changamoto ambazo zinapaswa kumulikwa zaidi ni hizi zifuatazo:

1) Muingiliano wa majukumu na wingi wa mamlaka za udhibiti katika kuidhinisha na kutoa hati, vibali na vyeti kwenye shughuli za uwekezaji na biashara. Katika kutatua changamoto hii tunapendekeza matumizi sahihi ya TEHAMA inayounganisha huduma za taasisi mbali mbali mahususi ili kupunguza ukubwa wa changamoto hizi na kuboresha huduma kwa wadau.
2) Urahisishaji wa upatikanaji wa taarifa zinazohusiana na fursa za uwekezaji utajenga mazingira rafiki na yenye kuchochea uwekezaji mpya. Tunapendekeza uanzishwaji wa daftari la kielekroniki litakalowezesha upatikanaji wa taarifa za uwekezaji kwa urahisi zaidi kuliko ilivyo sasa.

3) Kurahisisha mchakato wa kuhamisha biashara (TIN number) kutoka mkoa mmoja hadi mwingine. Kwasasa, uratibu wa mchakato huu hauko rafiki kwa mteja hivyo huhatarisha uhai wa biashara au ukwepaji wa kodi. Tunapendekeza mchakato huu uweze kufanywa kielektroniki ili kuongeza ufanisi wake.
4) Hali ya amani na utulivu nchini ni nyenzo madhubuti ya kuvutia wawekezaji na kuongeza mapato ya nchi. Aidha, ripoti mbali mbali mfano ripoti ya uhalifu na hali ya usalama ya mwaka 2020 ililitaja jiji la Dar es Salaam kama eneo lenye hali ya juu ya uhalifu "CRITICAL". Tunapendekeza uimarishwaji wa hali ya usalama kwa kutumia TEHAMA mamboleo katika kuzuia na kutambua matukio ya kihalifu.
5) Kupanua wigo wa taarifa zitokanazo na matumizi ya mashine za kielektroniki za kodi (EFD) ziweze kuwanufaisha walipa kodi kwa kuhifahdi taarifa za ulipaji kodi. Hii itaongeza ufanisi katika uhifadhi wa kumbukumbu zinazoakisi uhalisia wa mapato na mwenendo wa biashara husika.

c) Sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta muhimu zinazochangia pato kubwa la taifa. Yafuatayo ni mapendekezo ya namna inavyoweza kuchochea tija katika sekta hii.

1) Matumizi yakinifu ya TEHAMA katika sekta ya utalii yanaweza kuongeza tija na mapato. Ili kuongeza tija katika sekta ya utalii kupitia TEHAMA tunapendekeza kuongeza muonekano "visibility" ya vivutio vya kitalii kupitia mitandao ya intaneti. Sambamba na hilo, juhudi ziongezwe katika kuongeza upatikanaji wa maudhui ya ndani zinazoweza kuitangaza Tanzania kimataifa na hatimaye kuongeza mapato ya utalii.
2) Tunapendekeza kuongeza ufanisi wa kanzindata ya taarifa za watalii wanaotembelea vivutio vya ndani ili kuwezesha kuvutia watalii wapya kupitia wavuti na mitandao ya kijamii. Hali kadhalika, uchakataji wa taarifa za utalii kwa kutumia TEHAMA mamboleo utasaidia kuongeza ufanisi wa mipango mikakati ya kuimarisha vivutio vyetu na masoko ya bidhaa za utalii.
3) Pamoja na kupungua kwa matukio ya ujangili wa wanyama pori katika miaka ya karibuni, tunazidi kupendekeza kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ulinzi na ufuatiliaji wa wanyapori ambao ni rasilimali kuu ya utalii.

d) Matumizi ya kimkakati ya TEHAMA yataleta tija katika sekta ya kilimo na mifugo. Yafuatayo ni mapendekezo ya THTU ya namna TEHAMA inavyoweza kuchochea tija katika sekta hii:

1) Kuboresha uratibu wa mifumo ya taarifa mbalimbali ikiwemo masoko, bei, hali ya hewa na pembejeo kwa wakulima kupitia mifumo ya kielektroniki. Hii

itaondoa unyonyaji unaofanywa na madalali (middlemen) kwenye soko la mazao, na kuboresha matokeo ya kilimo.

2) Kutumia mifumo ya TEHAMA kuboresha upatikanaji wa pembejeo zenye ubora unaokubalika kwa ajili ya matokeo bora ya uzalishaji.
3) Uanzishwaji wa minada ya mazao kupitia majukwaa rasmi ya kielektroniki (e-auctions platforms). Hii itaongeza wigo, ushindani na uwazi katika ununuzi wa mazao ya kilimo na mifugo na kuongeza kodi inayopatikana na sekta ya kilimo na mifugo.
4) Kutumia mifumo ya kielektroniki katika kuboresha miundombinu ya maghala bora ya kuhifadhia mazao mbalimbali na kuanzisha stakabadhi za kielektroniki ya mazao ghalani. Hii itasaidia kuwawezesha wakulima kuwa na ufanisi zaidi ikiwa na pamoja na kukidhi vigezo vya kukopesheka. Vile vile uwepo wa mifumo madhubuti ya taarifa kuhusiana na mazao na maghala. Hili litavijengea vyama vya ushirika uwezo wa kutafuta masoko ya mazao ya wakulima ndani na nje ya nchi.
5) Kutumia data za satelaiti hususani takwimu za uchunguzi wa dunia (Earth Observation) katika kuchakata taarifa zinazohusu ufuatiliaji wa ukuaji na uzalishaji wa mazao ya kilimo ili kuweza kuwa na makisio sahihi ya uzalishaji na kuweka mipango mikakati thabiti mfano kuwaunganisha wakulima wadogowadogo na soko la uhakika. Hali kadhalika, matumizi ya data na TEHAMA mamboleo yanaweza kuongeza ufanisi wa kuwaunganisha wakulima na wataalamu wa kilimo kwa lengo la kuchagiza uzalishaji kitaalamu.

e) Sekta ya maji ni muhimu na wezeshi katika ukuaji wa sekta nyingine muhimu za uchumi, lakini sekta hii bado inakumbwa na changamoto nyingi ikiwepo usimamizi usio madhubuti wa mapato, ujenzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji na miundombinu yake. Tunapendekeza yafuatayo ili kuongeza tija katika sekta hii muhimu.

1) Kuongeza matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika kusimamia vyanzo vya maji, ikiwemo mifumo ya kulinda, kufuatilia na kubaini upotevu wa rasilimali maji pamoja na ubora wa viwango vya maji katika vyanzo.
2) Kuimarisha uthabiti wa matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika ukusanyaji na usimamizi wa mapato yatokanayo na usambazaji wa huduma za maji.
3) Tunapendekeza matumizi ya mifumo ya kielekroniki ya kuchakata data kwa ajili ya kuratibu mipango ya usimamizi wa maji ili kuimarisha huduma kwa namna bora zaidi.
4) Tunapendekeza matumizi ya data na takwimu mbalimbali sambamba na mifumo ya TEHAMA kuchakata uwezekano wa kuibua vyanzo vipya vya maji kwa ajili ya sehemu kame ili kuimarisha shughuli za uzalishaji.

f) Kuboresha makusanyo na usimamizi wa mapato na matumizi katika sekta ya afya. Katika eneo hili, THTU inapendekeza yafuatayo:

1) Juhudi zaidi zielekezwe kwenye kuziunganisha hospitali na vituo vya afya katika kuongeza ukusanyaji wa mapato yatokanayo na huduma za afya. Hospitali nyingi ziunganishwe na mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa mapato. Sambamba na hilo, THTU inapendekeza uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA inayohusika na ukusanyaji wa mapato katika hospitali ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa huduma za afya kuliko ilivyo sasa ambapo kuna mifumo zaidi ya mmoja inayotumika katika hospitali mbali mbali za umma.
2) Tunapendekeza uimarishaji wa kanzidata ya taarifa za wagonjwa nchi nzima ili kuimarisha ufanisi na kuwasaidia matabibu kutumia historia sahihi za wagonjwa. Hii itasaidia kuimarisha afya ya nguvu kazi na kupunguza gharama za matibabu yasiyo sahihi. Hali kadhalika, kanzidata hii itasaidia uimarishwaji wa mipango mikakati ya kukabiliana na magonjwa ya milipuko na kuboresha upatikanaji wa taarifa kwa ajili ya tafiti mbalimbali.
3) Usimamizi wa mnyororo wa usambazaji wa madawa uzingatie matumizi madhubuti ya TEHAMA ili kupunguza upotevu wa madawa na kuboresha upatikanaji wa dawa na uandaaji wa maoteo sahihi ya madawa yanayotolewa kwa hospitali za umma kuliko ilivyo sasa. Hii itasaidia kudhibiti ubora wa dawa na vifaa tiba vinavyotumika nchini.
4) Tunapendekeza Bohari kuu ya dawa (Medical Store Department) ijenge kanzidata na mfumo jumuishi wa kielektroniki unaohuisha data kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili kuboresha ufanisi wa ununuzi wa madawa ili kuepuka uagizaji wa madawa usio sahihi. Hii itasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira pamoja na gharama kubwa zitokanazo na uteketezaji wa madawa yanayofikia muda wa mwisho wa matumizi kabla ya kutumika.

g) Sekta za Nishati na Madini ni miongoni mwa sekta ambazo zimesimamiwa vizuri na serikali ya awamu ya tano. Tunaipongeza serikali kwa kazi nzuri inayofanyika katika sekta hizi. Aidha, THTU inapendekeza maboresho yafuatayo:

1) Upatikanaji wa taarifa za masoko na bei za madini. Hii itasaidia ushindani wa sekta ya madini kitaifa na kimataifa. Tunapendekeza uanzishwaji wa jukwaa rasmi la kielektroniki litakalotoa taarifa hizi muhimu kwa wadau wa madini.
2) Matumizi ya TEHAMA mamboleo katika kuboresha upatikanaji wa nishaji kwa gharama nafuu (Planning and Management of Grids and Microgrids).

3) Matumizi ya TEHAMA mamboleo katika kuboresha uzalishaji na usambazaji wa umeme (Smart-grid), hali kadhalika intelijensia ya uzalishaji unaokidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye (demand and supply forecasting).

h) Halmashauri za manispaa na majiji kitakwimu zimeendelea kuimarika katika makusanyo ya mapato kila mwaka. Walakini bado upo kwenye mbinu zinazotumika kufanya makisio ya mapato na utekelezaji wa mipango ya ukusanyaji mapato. Tunaamini zipo fursa za kuimarisha ukusanyaji huu zaidi kwa kuongeza ufanisi wa makisio na makusanyo kwa kufanya yafuatayo:

1) Tunashauri maafisa masuuli kuendelea kutumia wakandarasi na watoa huduma wanaotumia mashine za kielektroniki za kukusanya mapato na ambao wana kumbukumbu safi za kulipa kodi kutoka TRA. Kuanzisha utaratibu mzuri kwa wafanyabiashara wadogo kwa kuwawekea kodi ya zuio wanapotoa huduma kwa taasisi za serikali.
2) Kuongeza matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kuchakata takwimu katika kupanga na kutekeleza mipango ya makisio, ukusanyaji na usimamizi wa mapato kwa weledi zaidi.
3) Kuongeza uwazi wa miundo ya kodi kwenye kila ngazi ili kuondoa sintofahamu kwa walipa kodi na kuondoa mianya ya rushwa zitokanazo na kodi na kuongeza ulipaji kodi bila shuruti. Mifumo ya kielektroniki itaongeza ufanisi kwa sehemu kubwa ikitumika ipasavyo.

i) Ardhi ni rasilimali muhimu ya uchumi, hivyo ni vema ikasimamiwa kwa weledi ili kuwa na tija katika pato la nchi. Tunapendeza ongezeko la matumizi ya kimakakati ya TEHAMA mamboleo ili kuongeza ufanisi wa kupanga miji na kupunguza ukuaji holela wa miji ambayo hugharimu serikali fedha nyingi kulipa fidia pindi mipango miji inapofanywa kwa kuchelewa. Hali kadhalika upangaji wa miji wa mapema utaongeza dhamana ya wananchi katika kukopeshwa na taasisi za fedha na pia kuvutia uwekezaji.

Aidha matumizi ya TEHAMA mamboleo pamoja na data za satelaiti za uchunguzi wa dunia (Earth Observation) katika kukusanya na kuchakata data za ardhi na majengo zitasaidia kubaini makisio ya makuzi ya miji na matumizi ya ardhi. Hii itasaidia mamlaka husika kupanga kwa weledi mipango mikakati inayohusu na kuongeza vyanzo vya mapato na ufuatiliaji wake.

## 12. Hitimisho

THTU tunaishukuru serikali kwa kuendelea kuthamini mchango wa wafanyakazi katika kukuza uchumi wa taifa na maendeleo kwa ujumla, tumeshuhudia hatua mbali mbali

zimechukuliwa katika kuboresha maisha ya wafanyakazi na maslahi yao kupitia uboreshaji wa miundombinu na maboresho ya sehemu za kufanyia kazi ikiwemo ajira mpya. Pamoja na hayo bado tunaisihi serikali yetu pendwa kuendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na nyongeza ya mishahara ili kuwapatia motisha zaidi na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi kuelekea kujenga uchumi imara zaidi na wenye fungamanisho na maendeleo ya watu.

## 13. Rejea na Bibliografia


Chama cha Mapinduzi. (2020). "Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020." CCM Makao Makuu. Dodoma.

Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania. (2019). Ripoti ya Kamati ya Uchambuzi na Ushauri Kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2019/2020. THTU Makao Makuu. Dar Es Salaam. Desemba 2019.

Economic and Social Research Foundation. (ESRF). *Darubini ya Dira ya taifa 2025*.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2017). Ripoti ya Takwimu za Kodi 2015/2016. Tanzania Bara. Wizara ya Fedha na Mipango. Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS). Agodti 2017.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2018). Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022-202/2025.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2020). Faharisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Oktoba 2020. Maelezo ya Mbinu na Kanuni za Ukokotoaji Fahirisi za Bei za Taifa. Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS). Novemba 2020.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2020). Kodi na Shuru Mbalimbali kwa Mwaka 2020/2021. Wizara ya Fedha na Mipango. Mamlaka ya Mapato Tanzania- TRA. Julai 2020.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2021). "*Hotuba Ya Mheshimiwa Dkt. Philip I. Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Akiwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/22*." Wizara Ya Fedha Na Mipango. Dodoma. Februari 2021.

Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania. (2021). "*Maelezo ya Mhe. Dkt. Philip I. Mpango (Mb), Waziri wa Fedha ya Mipango, Akiwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Kiwango cha Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22*". Wizara ya Fedha na Mpango. Dodoma. Februari 2021.

Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania. (2021). "*Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22."* Wizara Ya Fedha Na Mipango. Dodoma. Januari 2021.

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. (2000). Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

National Cyber Security Index, “130. Tanzania, United Republic of 12.99,” 2021.

OSAC, “Tanzania 2020 Crime & Safety Report,” 2020.

Policy Forum. (2017). Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II): Ni kwa Jinsi gani Tutaboresha Utekelezaji katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa?. Kikundi Kazi cha Tawala za Mitaa (LGWG) cha Policy Forum. Jamana Printers. Novemba 2017.

United Republic of Kenya. (2018). Income Tax Act, 1975 as Ammended in 2018.

Ventures Sahara, “Towards Digital Economy in Tanzania.” 2019.

**Sheria mbalimbali za Kodi**

Sheria ya bajeti, Sura ya 439
Sheria ya Usimamizi wa kodi, Sura ya 438.
Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399.
Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332.
Sheria ya Ushuru wa Stampu, Sura ya 189.
Sheria ya Tozo za huduma za Bandari, Sura ya 264.
Sheria ya Magari (Kodi, Usajili na uhamishaji), Sura ya 124.
Sheria ya Tozo za viwanja vya ndege, Sura ya 365.
Sheria ya Tozo za huduma za bandari, Sura ya 264
Sheria ya michezo ya kubahatisha, Sura ya 41.
Sheria ya Elimu ya mafunzo ya Ufundi, Sura ya 82.
Sheria ya Tozo za usafirishaji magari ya kigeni, Sura ya 84.
Sheria ya kodi ya ongezeko la thamani, Sura ya 148.
Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020.
Sheria ya Marekebisho Anuwai ya Sheria zilizoandikwa za mwaka 2020.
Sheria ya Usimamizi wa forodha kwa jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004.
Sheria ya Usimamizi wa ushuru wa forodha kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (Marekebisho) yam waka 2011.
Sheria ya Ushuru wa barabara na mafuta, Sura ya 220.